

# Uzazi wa mpango...?

## Tafadhalii angalia uwezekano wa kupata kipimo cha mbeba kwa matatizo ya kijeni ya damu

### **Matatizo ya Damu ya Kijeni**

Takriban mtu \*1 katи ya watu 20 duniani kote inadhaniwa kuwa wamerithi jeni iliyobadilishwa ya globini ambayo wanaweza kuambukiza kwa watoto wao. Hii inaweza kusababisha shida ya damu ya kijeni, inayoathiri utengenezaji wa himoglobini. Himoglobini ni protini katika damu ambayo hubeba oksijeni kuzunguka miili yetu.

Matatizo haya ya damu ya kurithi hupitishwa kutoka kwa mzazi hadi kwa mtoto katika jeni. Jeni hubeba taarifa kuhusu sifa za binadamu kama vile rangi ya macho, rangi ya nywele na himoglobini.

**Matatizo haya ya damu ya kijeni yanarithiwa.**

**Matatizo haya ya damu ya kijeni hayaambukizi.**

**Matatizo haya ya damu ya kijeni hayasambazwi na vijidudu.**

Wakati mwagine mabadiliko hutokea kwa jeni, na kusababisha hali ya matibabu. Jeni za globini hubeba taarifa kwa watu binafsi kutengeneza himoglobini, hata hivyo mabadiliko katika jeni za globini yanaweza kusababisha yafuatayo.:

- **Beta thalassemia kuu** - anemia kali inayohitaji matibabu ya muda mrefu, ikiwa ni pamoja na utoaji damu mishipani kila mwezi.
- **Alpha thalassaemia** - aina moja inaweza kusababisha kifo kwa mtoto na hatari kwa mama wakati wa ujauzito.
- **Ugonjwa wa seli mundu** - hali ambayo inaweza kuhitaji kuongezewa damu mara kwa mara. Vizuizi vya uchungu sana vya mishipa ya damu hutokea katika maisha yote kutokana na mabadiliko katika umbo la chembe nyekundu za damu.
- **Himoglobini E** - kwa kawaada ni hali bila shida, lakini ikiwa imerithiwa na beta thalassemia au seli mundu, inaweza kusababisha hali mbaya inayohitaji matibabu ya muda wa maisha mzima.

### **Afy ya watu wanaobeba jeni iliyobadilishwa na globini**

Mtu anayebeba jeni iliyobadilishwa ya globin huitwa 'mbeba'. Mbeba ana afya. Ni muhimu kwamba daktari wake anajua kuwa yeye ni mbeba na kuweza kuzuiwa na kudhibitiwa na dawa.

### **Inamaanisha nini mtu anapokuwa mbeba wa jeni iliyobadilishwa ya globini?**

Ikiwa wewe ni mbeba wa jeni iliyobadilishwa ya globini ni muhimu kwamba mpenzi wako awe na kipimo cha damu ili kujua hali yake ya kuwa mbeba au la. Ikiwa ninyi wawili **wote** tu ni wabebaji wa mabadiliko fulani ya jeni ya globin ambapo mna hatari ya kupata mtoto aliyeathiriwa na matatizo ya damu ya kijeni.

### **Sababu za kupanga uzazi**

Jeni za matatizo haya ya damu ya kijeni yanaonekana sana kwa watu wa asili ya Mediterania, Mashariki ya Kati, Afrika (pamoja na Karibea au Mwfafrika wa Merekani), na pia nchi yoyote ya Asia: Uhindi, Pakistani, Sri Lanka, Bangladesh, Indonesia, Ufilipino, Thailand, Vietnam na Uchina n.k. Asili nyingine ni pamoja na Visiwa vya Pasifikasi na Wamaori wa New Zealand.

Wanandoa wanaopanga kuwa na familia, au ambapo mwanamke tayari ni mjamzito, wanapaswa kuzingatia kupima damu ili kuona kama ni wabebaji ikiwa walizaliwa au wana familia (hata jamaa wa mbali) kutoka mojawapo ya maeneo yaliyoordheshwa hapo juu. Kipimo hiki kinahitajika ili kubainisha uwezekano wa waathirika kuwa na mtoto aliyeathiriwa na ugonjwa wa damu ya kijeni.

Wale walio katika hatari ya kuwa na mtoto aliyeathiriwa wana chaguzi. Hali hizi zinaweza kutambuliwa mapema kama wiki ya 12 ya ujauzito. Uondoaji wa ujauzito unaweza kuzingatiwa, ikiwa unafaa. Watu wanaweza kuasili mtoto au kuzingatia mbinu za usaidizi za uzazi (kama vile matumizi ya mayai ya wafadhili au manii ya wafadhili). Wengine wanaweza kuchagua kuchukua bahati ya kuwa na mtoto aliyeathiriwa. Chaguzi hizi zote zinaweza kujadiliwa na Mshauri wa Jenetiki.

Upimaji unaweza kupangwa na daktari wa eneo lako au kwa kuwasiliana na hospitali zilizoordheshwa mwishoni mwa kijitabu hiki.


### **Taarifa muhimu kwa familia yako**

Ikiwa wewe au mwenzi wako ni wabebaji wa jeni iliyobadilishwa ya globini, wanafamilia wengine wanaweza pia kuwa wabebaji na wako katika hatari ya kupata watoto walio na ugonjwa mbaya wa damu. Inapendekezwa kwamba wanafamilia wengine wote na wenzi wao wapimwe hali ya mbeba kabla ya kupata watoto wao wenyewe.

## Uwezekano wa kupata mtoto aliyeathiriwa na ugonjwa wa damu ya kijeni


### Kielelezo 1:

Wazazi wote wawili ni  
wabebaji



### Kielelezo 2:

Mzazi mmoja tu ndiye mbeba



Kwa **kila** ujauzito, wanandoa hawa wana:

- Nafasi 1 kati ya 4 ya kupata mtoto anayerithi
- Nakala 2 za kawaida za jeni la globini na ni asiyebeba.
- Nafasi 2 kati ya 4 ya kuwa mbeba mwenye afya, kama wazazi wake. Mtoto huyu ana nakala moja ya kawaida ya jeni ya globini na nakala moja iliyobadilishwa ya jeni ya globini.
- Nafasi 1 kati ya 4 ya kupata mtoto ambayo anaweza kuwa na ugonjwa mbaya wa damu ya kijeni. Mtoto huyu amerithi nakala 2 zilizobadilishwa za jeni la globini.

Kwa **kila** ujauzito, wanandoa hawa wana:

- Nafasi 2 kati ya 4 ya kupata mtoto anayerithi
- Nakala 2 za kawaida za jeni la globini na asiyebeba.
- Nafasi 2 kati ya 4 ya kupata mtoto ambaye ni mbeba wa afya - kama mzazi wake. Mtoto huyu ana nakala moja ya kawaida ya jeni ya globini na nakala moja iliyobadilishwa ya jeni ya globini.

\*Kumbuka: (kum:  
Modell B, Darlison  
(2008) Global  
epidemiology of

haemoglobin disorders na viashiria vya huduma  
vinavyotokana - Taarifa ya World Health  
Organisation Vol 86, namba 6, Juni 2008: 417-  
496)



**Thalassaemia and  
Sickle Cell Australia**  
*Unifying Support and Genetics*

Thalassaemia and Sickle Cell Australia  
Moorleigh Community Village  
92-94 Bignell Road  
Bentleigh East  
VIC, 3165, Australia

Simu : +61 3 7015 5637  
Barua pepe:  
info@tasca.org.au